

Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala Manispaa ya Singida wapatiwa semina kuhusiana na zoezi la kitaifa la anwani za makazi

Halmashauri ya Manispaa ya Singida leo tarehe 23, Februari, 2022 imefanya mafunzo ya siku moja kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala kuhusiana na zoezi la uandaaji anwani za makazi katika Manispaa ya Singida.

Aidha wajumbe hao pia wameweza kupitia mpango kazi wa utekelezaji wa zoezi la anwani za makazi uliowasilishwa na timu ya uratibu ya Manispaa.

Pamoja na mafunzo hayo wajumbe hao pia waliweza kupewa elimu kwa vitendo katika moja ya mtaa katika Manispaa ili kujifunza namna ya kuweka namba kwenye nyumba kwa kuzingatia mtazamo wa mbele wa nyumba na pia mitaa inapoingiliana.



Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida Mhe. Yagi Kiaratu akiongoza wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala katika kufanya mazoezi kwa vitendo ya namna ya kuweka namba katika makazi kwa kuangalia miingiliano ya mitaa.



Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Utawala wakipewa maelekezo ya namna ya kweka anuani za makazi katika Mtaa wa Rwezaula, Kata ya Majengo Manispaa ya Singida. Anayetoa maelekezo ni Mkuu wa kitengo cha TEHAMA Ndg. Fadhili Mshamu



Waheshimiwa madiwani wa Kamati ya Fedha na Utawala Pamoja na wataalamu wakiwa katika zoezi kwa vitendo la kubainisha mitaa na namna ya kuweka namba katika nyumba/makazi na maeneo ya biashara